



## Ushirikishwaji na ulinzi wa watoto

Mlipuko wa Covid-19 umetupa wasiwasi sisi sote. Watoto wanakabiliana na shida zao za kipekee: maisha yao ya shulenii yamekatizwa, na wanafaa kwa sasa wakae makwao na kusomea huko. Mahusiano ya kila siku baina ya watoto yanayokuza kukua kwao yamesimama.

Kuna kanisa na viongozi mbalimbali wa jamii, washiriki na wafanyakazi wa Tearfund kuhusisha watoto katika mchakato wa maamuzi yao. Kufanyika kwa mambo haya yatawapa watoto nafasi ya kuchangia kwa jamii zao, pamoja na kuongeza kujiamini kwao.

Tunafaa tuzingatie vile tunavyozungumza na watoto kuhusu janga hili na kuwajali vipasavyo wakati huu.

Lengo la makala haya ni kutoa habari wazi na mwongozo katika kuhakikisha ushirika na ulinzi wa watoto wakati wa janga hili, ikijumuisha hali ambapo kuna mikakati ya kukaa mbali na watu na kufungiwa.

---

### Maswali muhimu

- Tutahusishaje watoto katika juhudii zetu za jamii na kanisa za kupambana na Covid-19?
- Tutahakikishaje kuwa watoto wanalindwa wakati huu?
- Ni kwa jinsi gani tutawasiliana na kujumuisha watoto?
- Tutakusanya viyi data katika mipango yetu kutambua mapengo yanayoweza kuwa katika kuwafikia watoto walio katika hatari zaidi?
- Tunaweza kusaidia jamii na kanisa kivipi ili kubadilisha mienendo yao kuhakikisha ulinzi na ushirika wa watoto wakati huu?



[tearfund.org/covid19](http://tearfund.org/covid19)



covid19-response-team@tearfund.org

## Tunawezaje kukabili?



### Kufahamu kanuni za kimsingi za ulinzi wa mtoto:

- Kuendeleza maslahi ya mtoto.
- Kustawi na kukua kwa mtoto ni muhimu.
- Usibague.
- Kuendeleza ushiriki wa watoto.



### Weka malengo ya kuhakikisha yafuatayo:

- Wasichana na wavulana wako salama wanakoishi, kusoma na kucheza.
- Watoto wanafikia bahari kama ujumbe wa afya ya umma na huduma muhimu.
- Utoaji wa huduma ni muhimu kwa mahitaji mbalimbali ya wasichana na wavulana.
- Hatari zinatambuliwa na kushughulikiwa (kwa mfano afya ya kiakili, dhuluma).
- Mifumo ya ulinzi wa watoto inaimarishwa.



### Badili kwa ujumuishi na ifaavyo:

- Hakikisha familia zilizo na watoto zinafikia rasilimali za afya na usafi.
- Zingatia mahitaji mahsusini ya watoto walemvu na walio na matatizo mengine ya kiafya.
- Husisha watoto katika mikutano ya kanisa na masomo ya bibilia yanayofanyika kwenye mtandao.
- Hakikisha kuna nafasi za watoto kutoa maoni (chanya na hasi) kuhusu changamoto wanazopitia watotot.



### Toa habari kuhusu masharti mapya kwa kuhusisha:

- Tumia jumbe zinazoleweka na watoto kuelezea maana ya masharti mapya na mabadiliko, kwa kutumia habari kutoka vyanzo vya kuaminiwa (kwa mfano Shirika la Afya Duniani)
- Hakikisha kuwa wazazi na walezi wanaelewa masharti haya.
- Hakikisha kuwa habari zinaeleweka na watu tofauti walio na mahitaji mbalimbali

## Rasilimali muhimu

Wakfu wa Asia: [COVIBOOK](#) (kitabu cha watoto kuhusu Covid-19 na Manuela Molina)

Mwongozo wa Dhuluma za Kijinsia: Covid-19: Jinsi ya kuhusisha watu walio hatarini

UNHCR: [Ulinzi wa mtoto](#)

UNICEF: Kitabu cha haki na usalama wa mtoto

Umoja wa Mataifa: Mkataba wa Haki za Mtoto

Serikali ya Irish Idara ya Elimu na ujuzi: Virusi vya Korona / rasilimali za Covid-19 (pamoja na bango zinazofaa watoto)

Unicef: Ugonjwa wa virusi vya Korona (COVID-19) kitovu cha habari.

*Rasilimali hii ilitafsiriwa kwa Kiswahili kwa msaada wa Translators without Borders.*

